



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAENDELEO YA MAFUNZO YA SENA YA WATU NA MAKAZI KATIKA NGAZI MBALIMBALI ZA UTAWALA.

TAREHE 28 JULAI, 2022

Ndugu Wanahabari,

Kama mnavyofahamu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na mafunzo ya Sena ya Watu na Makazi katika ngazi mbalimbali za utawala. Mafunzo hayo yanafanyika katika ngazi tatu ambayo yanajumuisha mafunzo kwa wakufunzi wa Sena ngazi ya Taifa; mafunzo kwa wakufunzi wa Sena ngazi ya Mkoa na Mafunzo kwa wasimamizi na Makarani wa Sena katika ngazi ya Wilaya.

Ndugu Wanahabari,

Napenda kutoa taarifa kuwa, mafunzo ya wakufunzi wa Sena wapatao 410 katika ngazi ya Taifa na wakufunzi wapatao 11,000 katika ngazi ya mkoa yamekamilika na washiriki walifaulu kwa kiwango cha juu kwa nadharia na kwa vitendo.

Ndugu Wanahabari,

Hatua inayofuata ni mafunzo kwa Makarani wa Sensa, Wasimamizi wa maudhui na wasimamizi wa TEHAMA wapatao 205,000 ambayo yatafanyika katika ngazi ya wilaya kuanzia **tarehe 31 Julai hadi tarehe 18 Agosti, 2022.** Washiriki wa mafunzo haya ni wale Watanzania waliokidhi vigezo na wenye sifa zinazohitajika ambao walikamilisha maombi ya nafasi hizo mtandaoni na waliofaulu kwenye usaili ambao ulifanywa na Kamati za Sensa za Wilaya na Kata **tarehe 19 hadi 21, Julai, 2022.**

Aidha, washiriki wengine wa mafunzo katika ngazi za Wilaya ambao watahiriki **kwa siku mbili za mwanzo, yaani tarehe 31 Julai, 2022 na tarehe 01 Agosti, 2022** ni Watendaji wa Kata wote nchini kwa Tanzania Bara na Masheha wote kwa Tanzania Zanzibar. Lengo la kuwashirikisha Watendaji Kata na Masheha katika mafunzo haya ni **kuwajengea uelewa zaidi kuhusu zoezi la Sensa ili waweze kwenda kusimamia shughuli zote za Sensa kwa ubora unaotakiwa na kuongeza kasi ya uelimishaji na uhamasishaji Sensa katika maeneo yao ya utawala.** Vilevile, itakuwa ni fursa ya pekee ya kuwapitisha kwa kina katika majukumu yao ya msingi ambayo wanatakiwa wakayatekeleze kabla ya kukamilika kwa mafunzo ya makarani na wasimamizi wa Sensa ikiwa ni sehemu muhimu ya kufanikisha zoezi la kuhesabu watu.

Ndugu Wanahabari,

Makarani na wasimamizi wa Sensa watakaofuzu mafunzo watakuwa na wajibu wa kufika katika maeneo ya kuhesabia watu watakayopangiwa siku mbili kabla

ya zoezi la kuhesabu watu, **yaani tarehe 21 na 22 Agosti, 2022** kwa ajili ya kutambua mipaka ya eneo la kuhesabia watu na kuhoji dodoso la jamii. Kisha watatakiwa kuendelea na zoezi la kuhesabu watu wote watakaokuwa wamelala ndani ya mipaka ya maeneo yao ya kuhesabia watu usiku wa kuamkia tarehe 23 Agosti, 2022. Zoezi la Kuhesabu watu litafanyika kwa takribani siku 6 likizingatia usiku wa kuamkia tarehe 23 Agosti, 2022 kama usiku wa wa rejea na siku 3 nyingine zitatumika kukusanya taarifa za Sensa ya Majengo.

Ndugu Wanahabari,

Kwa upande wa **Watendaji Kata na Masheha**, baada ya mafunzo watakayopatiwa kwa muda wa siku mbili, watakuwa na wajibu wa kushirikiana na Kamati za Sensa ngazi ya Kata kufanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha kuwa zoezi la Sensa linafanyika kwa ufanisi mkubwa katika maeneo yao ya utawala. Mambo ambayo wanatakiwa kufanya katika kipindi cha **kabla ya kuhesabu watu** yaani, kuanzia tarehe 03 Agosti, 2022 hadi usiku wa kuamkia tarehe 23 Agosti, 2022 ni pamoja na:-

- i. Kuongeza kasi ya uelimishaji na uhamashaji wa wananchi kushiriki Sensa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile redio za kijamii, ngoma, mikutano ya kijamii na kuwashirikisha Sekta Binafsi katika maeneo husika kushiriki kikamilifu katika zoezi hili la Kitaifa;
- ii. Kuainisha kaya za jumuiya kama vile hospitali, nyumba za kulala wageni, shule za bweni na nyingine ambazo zina uwezo wa kulaza watu 300 au zaidi ili uwekwe utaratibu maalumu wa kukusanya taarifa za Sensa katika kaya hizo;
- iii. Kuainisha maeneo wanapolala watoto/watu wanaoishi katika mazingira magumu (the homeless and street children);

- iv. Kuainisha makundi ya watu wanaohamama kama vile wafugaji na kambi za uvuvi (dago), kambi za wachuma karafuu, kambi za warina asali na wengineo;
- v. Kuainisha maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu kama vile vituo vikubwa vya usafiri (viwanja vya ndege, bandari, stesheni za treni na mabasi);
- vi. Kuhakikisha kuwa watu wote wanaoishi kwenye kambi za wakimbizi wanahesabiwa na wanahesabiwa mara moja tu ikiwa watakuwa wamelala ndani ya mipaka ya maeneo yao ya kiutawala usiku wa kuamkia siku ya Sensa; na
- vii. Kushiriki kikamilifu katika kutoa usafiri kama vile pikipiki, boti na vifaa vingine vinavyofanana na hivyo kwa lengo la kuwezesha zoezi la kuhesabu watu lifanyike kwa wakati na kwa ufanisi.

Vilevile, katika kipindi cha **wakati wa kuhesabu watu yaani tarehe 23 Agosti 2022** watendaji wa kata wote kwa kushirikiana na **wenyeviti na watendaji wa vijiji, mitaa na wenyeviti wa vitongoji** wote wanatakiwa kutoa ushirikiano wa kutosha kwa makarani wa Sensa ikiwa ni pamoja na kuwatambulisha kwenye kaya na kuratibu shughuli zote za kuhesabu watu katika maeneo yao.

Aidha, katika kipindi cha **baada ya kuhesabu watu kuanzia tarehe 01 hadi 06 Septemba, 2022** watendaji wa kata wote kwa kushirikiana na **wenyeviti na watendaji wa vijiji, mitaa na wenyeviti wa vitongoji wote** wanatakiwa kuhakiki idadi ya watu wote waliolala katika maeneo yao ya kiutawala kwa kupitia mfumo wa kidigitali watakaopatiwa kabla ya matokeo hayo hayajatangazwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Ndugu Wanahabari,

Nimalizie kwa kusema kuwa, upatikanaji wa Makarani na Wasimamizi wa Sensa Mwongozo ulitolewa na ulifuata vigezo vyote upatikanaji wa ajira na mchakato ulikuwa wa uwazi na umefanyika katika ngazi ya wilaya na Kata/Shehia zilihusika. Hivyo, rai yangu kwa Makarani na Wasimamizi ni kwamba watumie fursa hii vizuri wazingatie mafunzo yatakayotolewa darasani ambayo yatahusisha nadharia na vitendo. Kama ilivyokawaida ya mafunzo yoyote yale, Makarani na wasimamizi watakaoshindwa mitihani itakayotolewa kwa mujibu wa ratiba ya mafunzo wataondolewa mapema.

Hivyo, kila mmoja wetu anatakiwa kutimiza wajibu wake ili kuhakikisha Sensa ya Mwaka 2022 inakuwa ni Sensa ya mafanikio makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali,

Ofisi ya Taifa ya Takwimu,

Dodoma,

28 Julai, 2022.



